# Barua kutoka Taizé

n° 274 Toleo maalum SW

Kwa mara ya kwanza, moja ya mikutano yetu ya ulaya unafanyika Berlini. Berlini ni jiji lenye mchanganyiko mkubwa wa watu, jiji ambalo linaelekea mbele, lakini pia kujaribu kujumuisha kumbukumbu ya maumivu yaliyopita, jiji ambalo wakazi wake wameonesha kuwa hawatakatishwa tamaa kwa vipindi vigumu. Ingawa wachache, wakristu wanajaribu kuiishi injili. Kwa kuwa wanatoka madhehebu tofauti, ushirikiano na kujumuika bila kujali madhehebu si hiyari bali lazima. Makanisa na parokia nyingi zimekuwa sehemu za mshikamano ambapo wahitaji wanakaribishwa.

Ziara ya kwanza ya mabruda wa Taizé mjini Berlini ilikuwa mwaka 1955. Ulipojengwa ukuta na kuugawa mji katika vipande viwili mwaka 1961, mabruda waliongeza ziara za kuelekea Berlini mashariki. Miaka ya 1980 vikundi vingi vilianzishwa huko. Bruda Roger alikwenda kwenye hatua ya safari ya imani mwaka 1986. Ililazimu kuomba ruhusa kutoka kwenye utawala wa Kikomunisti kufanya sala, ambayo ilifanyika kwa wakati mmoja katika makanisa makubwa mawili, ya Kikatoliki na Kiprotestanti, kuleta pamoja vijana 6000 kutoka Ujerumani mashariki. Ruhusa ilitolewa kwa masharti kuwa hakuna washiriki kutoka magharibi. Sasa kipindi hicho kimekwisha na Berlini ni ishara duniani kote kwa wale wote ambao, wanajaribu kuvuka mipaka ya utengano ili kusambaza imani.

BARUA 2012

## Kuelekea mshikamano mpya

Kwa msikamano mpya kati ya binadamu kuchipuka katika ngazi zote- kwenye familia, jumuiya, miji na vijiji, kati ya nchi na mabara- maamuzi thabiti yanahitajika.[1]

Utambuzi wa changamoto na maumivu yanayotukabili binadamu, na dunia kusitupe uwoga na kukata tamaa.[2]

Na pia matumaini ya binadamu daima yanakabiliwa na changamoto. Ugumu wa kiuchumi ambao unaongeza mzigo, wakati mwingine ugumu wa mahusiano ya kijamii, na hisia ya kukosa msaada wakati wa mahafa hujaribu kuharibu miche ya imani.[3]

Ili kutengeneza njia mpya za mshikamano, je ni muda sasa kufanya bidii za kuchimbua vyanzo vya imani?

Pale imani iliposalitiwa, vidonda huacha alama ndani sana.

Imani si kuamua kwa upofu, wala si neno rahisi. Ni matokeo ya uamuzi, ni tunda la mvutano wa ndani. Kila siku tunataitwa kupiga hatua mbele kuelekea kuamini na kuacha uwoga.

### IMANI KATI YA BINADAMU

Kufungua njia za imani ni kuitikia hitaji muhimu: ingawa mawasiliano yamekuwa rahisi zaidi, jamii zetu zinaendelea kubakia kuwa zimegawanyika.

Kuta zipo siyo tu kati ya watu na mabara, lakini pia karibu na kwetu, na hata katika moyo wa binadamu.

Fikiria imani zilizojengeka kuhusu mataifa mengine. Wafikirie wahamiaji, wako karibu na mara nyingi wako mbali sana. Dini bado hazifahamu chochote kuhusu dini nyingine, na Wakristu wenyewe wamegawanyika katika madhehebu mengi.

Amani duniani huanzia mioyoni mwetu.

Kuanzisha mshikamano, tunahitaji kuwaendea wen-

1 Ingawa mshikamano kati ya binadamu umekuwa muhimu, daima kunahitajika kuamshwa na kuelezwa kwa njia mpya. Leo pengine kuliko nyakati nyingine katika historia, ni vyema kwa kizazi kipya kutafuta njia za kushirikishana rasilimali za dunia kwa haki, katika kugawanya mali, kwa usawa zaidi baina ya mabara na ndani ya nchi.

2 Inawezekana kuvuta kasi kuelekea mshikamano mpya. Kuvuta kasi huku inachochewa na imani kuwa historia ya ulimwengu inaendelea kuandikwa. Tujikumbushe mifano michache, ikiwemo; Baada ya vita ya pili ya dunia, wanasiasa wachache, waliamini bila kukatishwa tamaa kuwa maridhiano yanawekana, na kwa moyo kuanza kuijenga Ulaya kwa mshikamano; mwaka 1986 mapinduzi ya amani yalileta mabadiliko makubwa Ufilipino; muungano wa wananchi wa Polandi Solidarność uliandaa, na bila umwagaji wa damu, njia ya kupata uhuru kwa nchi nyingi za Ulaya; kuanguka kwa ukuta wa Berlini mwaka 1986 miaka michache kabla kutokea isingeweza kufikirika; wakati huo huo, nchi za Amerika ya kusini zilipiga hatua kuelekea demokrasia na kuanza kupata maendeleo ya kiuchumi, ambayo yanatia matumaini kuwa kila masikini anaweza kunufaika nayo bila kuchelewa; mwisho wa utawala wa kibaguzi nchini Afrika ya Kusini na Nelson Mandela kunyoosha mkono kupelekea maridhiano hata zaidi ya matarajio; hivi karibuni tumeshuhudia mwisho wa mapigano ya kisiasa katika Ireland Kasikazini na nchi za Basque.

3 Matatizo ya uchumi wa dunia yanatupa maswali mengi. Uwiano wa kisiasa na nguvu za kiuchumi baina ya nchi na mabara unabadilika. Tofauti za kipato zinaongezeka. Hazina ya jana haina maana tena leo. Je, hii inaweza kuwa sababu ya kutafakari maamuzi tunayoyafanya katika maisha yetu?

gine, wakati mwingine mikono mitupu, kumsikiliza na kumwelewa mwanamke au mwanaume ambaye anafikiria tofauti nasi... tayari tukio gumu laweza kuanza kutatuliwa.

Tujaribu kuwa waangalifu na wasikivu kwa wanyonge, wale ambao wanashindwa kupata kazi... usikivu wetu kwa walio masikini waweza kuonyeshwa kwa aina ya shughuli za kijamii. Kwa undani, huu ni mtazamo wa uwazi kwa wote: wale walio karibu nasi na, hususani wale walio masikini wanaotuhitaji.[4]

Kwenye kukumbana na umasikini na kukosa haki, wengine hufikiria vurugu au hata kushawishika kufikiria mapigano yasiyo na mwelekeo. Kumwaga damu hakuwezi kuwa njia ya kubadilisha jamii.[5] Lakini tunahitaji kuwasikiliza vijana wanaoonesha masikitiko ili kuelewa sababu za msingi.[6]

Kuvuta kasi kuelekea mshikamano mpya kunakuzwa na imani zilizo kina: hitaji la kushirikishana ni moja wapo.[7] Huu ni wito ambao unaweza kuwaleta pamoja waumini wa dini tofauti vile vile waamini na wasio waamini.

## IMANI KWA MUNGU

Mshikamano kati ya wanadamu waweza kupata msingi imara kwa kumtazama Mungu lakini mara nyingi kumwamini Mungu kwaleta mashaka, Waamini wengi wana uzoefu hasi katika sehemu zao za kazi au masomoni na mara nyingine katika familia zao.

Kuna watu wengi wanashindwa kuamini katika Mungu anayewapenda. Kuna wengine kwa ukweli mkubwa, wanauliza swali hili: ninawezaje kufahamu kama nina imani?

Leo hii imani inaonekana kama hatari, hatari ya kuamini.

Imani haimaanishi kwanza ya yote kushika ukweli, ni uhusiano na Mungu.[8] Inatuita kuugeukia mwanga wa Mungu.

Mbali na kutufanya wanyonge au kutushupaza kutimiza matazamio yetu[9], imani kwa Mungu inatufanya kuwa huru ¨uhuru kutoka , huru kuishi kwa kuwatumikia wale ambao Mungu ametukabithi.[10]

Imani kwa Mungu inavyo ongezeka, ndivyo mioyo yetu inavyofunguka kwa binadamu popote walipo duniani, na tamaduni zote. Mioyo yetu pia inaweza kukubali sayansi na teknolojia ambazo zinaweza kupunguza maumivu na kuwezesha jamii kuendelea.

Kama jua, Mungu anang'aa sana kumwangalia moja kwa moja. Lakini Yesu anawezesha mwanga wa Mungu kupitia kwake. Biblia yote inatuongoza kweye imani hii: Mungu apitaye kila kitu anaingia kwenye maisha ya binadamu na kuzungumza nasi katika lugha tuielewayo.

Je nini ni tofauti katika imani ya Kikristu? Yesu na uhusiano ulio hai pamoja naye. Hatuwezi kamwe kumaliza kulielewa hili.

## KRISTU WA UMOJA

Sisi ni wasafiri, tunaotafuta ukweli. Kuamini katika Kristu haimaanishi kuumiliki ukweli, bali kumwacha yeye, ambaye ni ukweli, kutuchukua na kutuongoza kuelekea ambako kuna muonekano wake kamili.

Kitu ambacho kitakuwapo daima na kutushangaza upya ni kuwa Yesu alitangaza mwanga wa Mungu kupitia maisha marahisi. Maisha matakatifu yalimfanya zaidi kuwa binadamu.[11] Kwa kujionyesha kikamilifu katika ura-

4 Umasikini si kuhusu mali tu. Kwaweza kuhusisha kukosa marafiki, kushindwa kupata maana ya maisha, kutoweza kupata ushairi, muziki, sanaa vyote vinavyoweza kutufungulia uzuri wa uumbaji.

5 Mwaka 1989 Ujerumani mashariki, kuamkia kudondoka kwa ukuta, waandaji wa maandamano waliwaomba watu kubeba mshumaa uliowashwa. Mkono mmoja ulihitajika kuubeba mshumaa na mwingine kuzuia upepo usiuzime, na hivyo kutokuwa na mkono ulio huru wa kufanya vurugu.

6 Vijana wa Uhispania walioshirki katika maandamano ya Indignatos mjini madrid waliniandikia; Chochote kinaweza kutokea kama mambo hayatakwenda sawa. Watu wengi hawana ajira; wanapoteza makazi yao na haki zao za msingi kama binadamu. Kuna hali ya kutoelewana na hasira ya mfumo mbaya wa sheria, uchumi na mfumo wa kijamii, demokrasia ya uwongo ambayo haimwakikishii mwananchi haki ambazo zimeandikwa kwenye katiba yetu, makazi sahihi, haki za kimwili na uadilifu wa kiakili.... Unatuuliza ni nini Taizé yaweza kutufanyia. Jibu letu: unaaweza kuendelea kufanya kile ambacho mnafanya, kutuonesha jinsi ya kutunza amani ya ndani. Tunahitaji sala zenu na hali yenu ya kuguswa na hali yetu. Na vile vile mnaweza kusaidia kusambaza taarifa kwe vijana wengine wanaoguswa na hali kama yetu.

7 Kutambua kwa mfano Nchi za magharibi haziitwi kutoa misaada ya kibinadamu kwa nchi za Afrika kama zinavyoitwa kuhakikisha haki inatendeka kwenye bara hilo. Yaweza kuwa sawa pia kwenye nchi nyingine kama Haiti: watu wa Haiti pamoja na imani yao halisi, wamekuwa kati ya watu waliodharirishwa sana katika historia.

8 Mara nyingi, Papa Benedikti XVI amesisitiza kuwa uhusiano binafsi na Mungu ni mwanzo wa imani, kwa mfano aliandika: kuwa mkristu si tokeo la uamuzi wa nidhamu au wazo la ajabu, bali ni mkutano na tukio, mtu, ambaye anayeyapa maisha wigo mpya na mwelekeo thabiti.(Benedict XVI, Deus caritas est, utangulizi na. 1)

9 Imani yetu inahitaji kusafishwa kila mara, kuondoa mitazamo migeni na uwoga, wakati mwingine kupitia mapigano ya ndani kati ya imani na mashaka. Akili yetu inashiriki katika vita hii na hairidhishwi kwa kuyashika tu yale tusiyoyajua. Ndio maana vijana wengine siku hizi hawaridhishwi kwa kupokea tuu kwa mapokeo ya Kanisa; kuamini, ushiriki binafsi na msukumo ni muhimu kwao.

10 Akizungumzia maneno ya mtume Paulo, Huru kwa kuheshimu wote, nimejifanya mtumwa wa wote(1 Wakoritho 9:19), Martin Luther aliandika: Kristu kwanza kabisa ni mtu huru, si mtumwa wa yeyote. Mkristu ni mtumishi mtiifu; ni mtumishi wa wote. (Luther, Uhuru wa Mkristu)

11 Yesu hakuwa mfanya mazingaombwe. Alifanya miujiza, haswa kuponya wagonjwa, lakini wakati ambapo angethibitisha kuwa yeye ni yule ambaye ametumwa na Mungu msalabani, kulikuwa na ukimya wa Mungu, ukimya ujulikanao kwa wote wanaoteseka na alikubali kuupokea. Ilikuwa vigumu kwa mitume kuelewa kuwa Yesu alikuwa masiha masikini. Yawezekana kuwa walitarajia kuwa angebadilisha hali ya kijamii na kisiasa za kipindi hicho, hawakutambua kuwa ilimpasa hasa kuuondoa uovu katika mizizi yake.

hisi wa maisha ya binadamu; ametuwezesha kuamini wanadamu. Kuanzia hapo hatuwezi tena kuchoshwa na ulimwengu au sisi wenyewe.

Kwa kukubali kifo ya mateso cha mateso bila kulipiza; Yesu alileta upendo wa Mungu pale palipo na chuki.[12] Msalabani, alikataa kukumbatia kifo na hali ya kutoguswa. Alipenda mpaka mwisho kabisa, licha ya maumivu kuwa na tabia ya kutoeleweka na ajabu, aliendelea kuamini kuwa Mungu ni zaidi ya uovu na kuwa kifo hakitakuwa na sauti ya mwisho. Kwa ajabu, mateso yake msalabani yakawa ishara ya upendo usiyo na kikomo.[13]

Na Mungu akamuinua kutoka mauti. Kristu si tu ni wa zamani; yuko kwa ajili yetu katika kila siku mpya. Anawasilisha Roho mtakatifu, ambaye anatuwezesha kuishi maisha na Mungu.

Kiini cha imani yetu ni Kristu mfufuka, aliyepo kati yetu, ambaye ana uhusiano binafsi wa upendo na kila mmoja. Kugeuza macho yetu kuelekea kwake kunaamsha mshangao na uelewa wa kina wa uwepo wetu.

Tunapoangalia mwanga wake katika sala, taaratibu mwanga wake unaanza kuangaza ndani mwetu. Fumbo la Kristu linakuwa fumbo la maisha yetu wenyewe. Utata wetu wa ndani na uwoga wetu vyaweza kubaki. Lakini Roho mtakatifu, Kristu anaingia kamili katika vile vinavyotuletea uwoga . Ili mwanga wake uangaze sehemu zenye giza ndani mwetu.[14]

Sala inatuongoza kwa Mungu na wakati huo huo kuelekea duniani.

12 "Alipotukanwa, yeye hakujibu tusi; alipoteseka yeye hakutoa vitisho, bali aliweka matumaini yake kwa Mungu ambaye anahukumu kwa haki.(1 Petro 2:23)

13 Tunapokumbana na maumivu yasiyoeleweka ya watu wasio na hatia mara nyingi tunahudhunika. Swali, na kilio ambacho kimesikika katika historia ya binadamu kinahusu mioyo yetu: Mungu yuko wapi? Hakuna majibu yaliyotayari, lakini tunaweza kujikabidhi kwa Kristu ambaye amekishinda kifo na ambaye yuko kwenye mateso yetu.

14 Sala, kutafakari mwanga wa Mungu pia ni kusikiliza, kupitia maandiko tunatambua kuwa Mungu ni yule anayeongea nasi na ambaye wakati mwingine anatuuliza. Na wakati mwingine, Kristu ni mtu masikini ambaye anataka kupendwa na ambaye anatuambia, Nasimama mlangoni na kubisha hodi (Ufunuo 3:20).

Kama Maria Magdalena ambaye, asubuhi ya Pasaka, alimwona Kristu akiwa hai, tunaitwa kuwashirikisha wengine habari hii njema.[15]

Wito wa Kanisa ni kuwakusanya katika amani ya Kristu wanawake, wanaume na watoto wa lugha zote, wa nchi zote, duniani kote. Kanisa ni ishara kuwa Injili inazungumza ukweli; ni mwili wa Kristu, unaoongozwa na Roho mtakatifu. Inafanya Kristu wa umoja kuwepo.[16]

Bila kuchoka kanisa linaposikiliza,[17] kuponya, na kupatanisha, linakuwa wakati ambapo linang'ara ¨muunganiko wa upendo na huruma, ni taswira halisi ya Kristu mfufuka. Kanisa laweza kufanya kuamini imani kuangaza katika mioyo yetu, kwa kutokuwa mbali, kutokuwa daima katika hali ya kujihami, kuwa huru kutoka vitu vyote vinavyoilemea.[18]

## KUJARIBU KUWA "CHUMVI YA DUNIA"

Kristu wa umoja hakuja kuwatenga wakristo na kuwajengea jamii tofauti kwa ajili yao; anawatuma kuwatumikia binadamu kama chachu ya imani na amani.[19] Umoja ulio wazi wa wakristu siyo lengo la mwisho bali ni ishara katika ubinadamu: wewe ni chumvi ya ulimwengu.[20]

15 Angalia Yohana 20:11-18.

16 "Kristu wa umoja ni msemo wa Bruda Roger. Hivyo hivyo mwana teolojia kutoka Berlini Dietrich Bonhoeffer, akiwa kijana wa miaka 21 aliunda msemo Kristu anayaishi kama jumuiya Aliandika kuwa, kupitia Kristu ubinadamu unaunganishwa kweli na Mungu."

17 Kila mahala katika Kanisa, utume wa kusikiliza waweza kufanywa kwa wanawake na wanaume ambao wanajitoa kikamilifu kwa hilo. Kama watu wa kawaida ambao wanaweza kusikiliza, kwa kusaidiana na watumishi waliosimikwa.

18 Bruda Roger, Peace in All Things

19 Ingaawa hii huduma inamaanisha kwenda kinyume na mkondo wa vyote ambavyo vinavyoondoa ubinadamu katika jamii, huku kunafanywa zaidi ya yote na daima kwa kuzingatia heshima na majadiliano yanayojenga, pamoja na tamaduni tofauti duniani na kuzingatia historia. Chachu haioneshi nguvu yake mpaka inapoletwa karibu kabisa na ngano, na siyo tuu karibu bali inapochanganywa mpaka unga na ngano haviwezi kutofautishwa (Mtakatifu Yohana Chryostom, Mahubiri 46 katika Mathayo).

20 Mathayo 5:13

---

## Vituo vifuatavyo katika safari ya imani Duniani

**Bruda Alois pamoja na vijana kutoka mataifa mbali mbali watakwenda Geneva, ijumaa Machi 2, 2012 kutembelea Baraza la Makanisa Duniani.**

**Mkutano wa tatu wa kimataifa wa vijana barani Afrika utafanyika Kigali, Rwanda, kuanzia Novemba 14 hadi 18, 2012.**

**Mkutano wa 35 wa vijana wa Ulaya utafanyika kuanzia 28 Disemba, 2012 hadi 2 Januari, 2013 mjini Roma Italia.**

**Pamoja na mabruda na vijana kutoka mabara mbali mbali, Bruda Alois atakwenda Istambul, Januari 4 hadi 6, 2013, kusherekea Epifania pamoja na Patriaki wa Constantinopol, Bartholomew I, na wakristu wa jiji hilo.**

Kwa msalaba wake na ufufuko Kristu ameunda mshikamano mpya wa binadamu wote. Ndani yake tayari ameshashinda migawanyiko yote ya makundi ya binadamu yanayopingana; ndani yake wote ni familia moja.[21] Upatanisho na Mungu unajumuisha upatanisho pamoja na binadamu.[22]

Lakini kama chumvi ikipoteza uchumvi wake.... Lazima itambulike kuwa sisi wakristu mara nyingi tunaupotosha huu ujumbe wa Kristu. Haswa, tutawezaje kuchochea upendo kama tutaendelea kugawanyika?

Tupo kwenye kipindi cha historia ambacho tunahitaji kuupa nguvu mpya huu ujumbe wa upendo na amani. Je tutafanya yote tuwezayo ili, kuwa huru kutoka kutokuelewana, hivyo kuweza kuangaza urahisi wake wa awali?

Je, bila kulazimisha chochote, kusafiri bega kwa bega na wale wasioshiriki imani yetu lakini wanatafuta ukweli kwa mioyo yao yote?[23]

Katika kujaribu kutengeneza njia mpya za mshikamano na kufungua njia za imani, kuna, na zitaendelea daima kuwepo, vikwazo. Wakati mwingine vinaweza kuonekana kana kwamba vinatuelemea. Kwa hiyo tufanyeje? Je, siyo jibu letu kwa matatizo yetu binafsi, na yale wanayopitia watu wengine, ni kupenda tena zaidi?

fr. Alois

21 Kristu alisema: Nitakapoinuliwa kutoka ardhini, nitavuta watu wote kwangu (Yohana 12:32). Na mtume Paulo: Hakuna tena Myahudi wala Mgiriki, mtumwa au aliye huru, mwanaume au mwanamke (Wagalatia 3:28).

22 Angalia Wafilipi 2:14 - 18. Kristu alibomoa ukuta utengao watu wa Mungu na wengine; wote wanauwezo wa kumfikia. Mshikamano hauwezi kuishia katika familia moja au nchi moja; waweza kuifikia zaidi ya vitu mahususi.

23 Kwa mfano kwa kushirikishana kuhusu maswali kama: Nini maana ya maisha yangu? Nini kinayapa mwongozo? Lengo gani linaunganisha pamoja uwepo wangu?

# Mwaka 2015: Kukusanyika kwa mshikamano mpya

**2012: Kufungua njia za imani katika binadamu.**

**2013: Kuchimbua chemichemi za imani kwa Mungu.**

**2014: Kutafuta muungano ulio wazi kwa wote wampendao Kristu.**

**2015: Kuwa chumvi ya dunia**

**Na, kurudia vipengele muhimu vya utambuzi huu na kushika kasi mpya,**

**Agosti 2015:**

## Taizé, mkusanyiko wa mshikamano mpya

**Miaka 75 ya kuanza kwa Jumuiya ya Taizé**
**Miaka 100 kumbukumbu ya kuzaliwa Bruda Roger**

**Hili vijana wengi iwezekanavyo waweze kusikilizwa, huu mkusanyiko utaandaliwa kwa mikutano katika kila bara.**

**Kwa miaka mitatu na nusu ijayo,safari yetu ya imani duniani itafuata njia za kufanyia kazi dhima za barua ya mshikamo mpya.**

**Mshikamano mpya ambao unaweza kuleta pamoja wasafiri wote wa amani, wasafiri wa ukweli, bila kujali kuwa waamini au la.**

**Miaka mitatu na nusu kuwezesha vijana kutoka kila bara kukusanya nguvu, kukusanya pamoja matamanio yao, mawazo na uzoefu wao.**

Directeur de publication : A. Trochard, Edition et impression : Ateliers et Presses de Taizé, 71250 Taizé, France, CPPAP n° 0115K79608 - DL 1135